GREDI YA TANO
KISWAHILI KAZI YA ZIADA
MASWALI

I. ***KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA*** *(Alama 5)*

1. ***Tunga sentensi ukitumia vitanzandimi vifuatavyo****.(alama 2)*
   a. *Kasa*
      _____
   b. *Kaza*
      _____
   c. *Saa*
      _____
   d. *Zaa*
      _____
2. ***Tegua kitendawili kifuatacho*** *(alama 1)*
   Bak bandika bak bandua
   _____
3. *Kamilisha methali zifuatazo (alama 2)*
   a. *Mtaka cha mvunguni* _____
   b. *Chanda chema* _____

II. *UFAHAMU (Alama 10)*

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mlolongo wa magari matano ulikuwa ukipita kwa utaratibu ambapo kando ya barabara, watu waliyatazama magari hayo kwa makini mno kutokana na jinsi yalivyopambwa kwa maua kochokocho.

Miongoni mwa wale waliojipanga barabarani kuyashuhudia hayo, alikuwa kijana Abdala. Ilikuwa ni siku ya Jumamosi alasiri. Gari la kwanza ambalo lilikuwa limepambwa zaidi, liliwabeba bwana na bi arusi.

a. *Ni magari mangapi yaliyotajwa katika kifungu hiki?*
   _____*(alama 1)*
b. *Watu walitazama magari wakiwa wapi?*
   _____ *(alama 1)*
c. *Ni nini kilichovutia macho ya watazamaji?*
   _____*(alama 1)*
d. *Taja mhusika mmoja kati ya walioshuhudia magari hayo*
   _____*(alama 1)*
e. *Eleza maana ya neno alasiri* _____ *(alama 1)*
f. *Tukio hili lilifanyika siku gani?*
   _____*(alama 1)*
g. *Gari la kwanza lilibeba akina nani?* _____*(alama 1)*
h. *Eleza aina ya nomino zifuatazo kama zilivyotumika katika kifungu hiki (alama 3)*